

# TAASISI YA USTAWI WA JAMII

Taasisi Ustawi  
Simu: 2700918/2774443  
Nukushi: 2701375  
Barua pepe: [info@isw.ac.tz](mailto:info@isw.ac.tz)  
Tovuti: [www.isw.ac.tz](http://www.isw.ac.tz)



S.L.P 3375  
Kijitonyama  
Dar es salaam

---

## TAARIFA KWA WANAJUMUIA/WADAU WA ISW

### TAHADHARI DHIDI YA VIRUSI VYA COVID-19 (CORONA)

Kijitonyama, Dar es Salaam, Machi 20, 2020,

Kufuatia janga la Dunia la kuenea virusi vya ugonjwa hatari COVID 19 CORONA Taasisi ya Ustawi wa Jamii imechukua hatua na inatoa maelekezo yafuatayo:-

1. Taasisi imefunga milango yote na kubakiza mlango mmoja (lango la barabara ya shekilango) ambao utatumika kuingia na kutoka eneo la Taasisi, aidha kila atakayeingia au kutoka atalazimika kuosha mikono yake na maji safi yenye dawa maalum au vitakasa mikono (Sanitizers) ambavyo vipo mlangoni.
2. Taasisi inawaelekeza wanafunzi wote ambao wapo likizo na ambao bado wanafanya tafiti (Research) wasifike kuwaona wasimamizi wao wa tafiti (Supervisors) na badala yake watawasiliana nao kwa njia ya baruapepe (e-mails).
3. Taasisi imesitisha huduma zote kwa wanafunzi (utoaji Vyeti/Transcript n.k) kwa sasa mpaka hapo itakapo tangazwa tena. Kwa msaada wa dharura yoyote tafadhali tuma ujumbe kwa barua pepe "info@isw.ac.tz" ama piga simu 0677 111 200 au 0735 50 90 90.
4. Taasisi itaendelea kutoa taarifa na maelekezo kwa Wafanyakazi na Wanafunzi kuhusu hatua za kujikinga na ugonjwa huu kadiri itakapobidi.

Imetolewa na;  
Ofisi ya Uhusiano- ISW